# MWAKA 2021 NI MWAKA WA KANISA KUWA MACHO (KUWA MAKINI SANA)
# Maandiko Neh 6: 10 – 13

1. **UTANGULIZI**

   Kuna aina mbili za macho

a) Macho ya mwili huu – **Math 6: 22 – 23**

b) Macho ya rohoni – ***2Wafalme 6: 16 – 17.***

- Daima watu tuko makini sana kulinda macho yetu ya mwili kwa sababu tunafahamu umuhimu wake; tunakula vyakula bora ili kulinda macho yetu kwa sababu tunafahamu fika kwamba macho yetu yakiharibika hatuwezi kufanya kazi zetu muhimu kama za kuendesha gari; kuchapa computer n.k.
- Kazi kubwa ya macho haya ya mwili Yesu aliieleza kwa makini kwamba ni taa ya mwili; ndiyo yanayoona hatari na kuepusha mwili wote na hatari hiyo; ndiyo yanayoona kitu kizuri na kuushawishi mwili ukipate; hata tamaa zote za mwili zinasababishwa na macho ziwe njema ama mbaya; woga wa mambo wengi ikiwa ni pamoja na woga wa maadui; woga wa Corona n.k vyote macho ya mwili yanahusika. Kwa kifupi macho haya ni ya muhimu sana, yanatufanya tusiwe tegemezi kwa watu wengine kutushika mkono na kutuongoza hata kwenda msalani na mambo mengine mengi.
- Ukitaka kujua zaidi umuhimu wa macho ya mwili jifunze kwenye taa za magari zilivyo muhimu sana wakati wa usiku; au taa za umeme nyumbani kwako zilivyo muhimu sana usiku; unaonaje zinapozimika ghafla!!!

*2.* Kama macho ya mwilini yalivyo muhimu na faida tele kwetu; macho ya rohoni ni muhimu zaidi kwa wana wa Mungu ili waweze **kuujua** ukweli halisi kuhusu Yesu Kristo na ufalme wake na majeshi yake. **Macho ya rohoni ndiyo yanayotupa ufahamu wa hali ya juu wa kuuona mpango wa Mungu halisi wa kumtoa mwanae Yesu Kristo ili atuokoe sisi tuliokuwa mateka wa ibilisi; macho ya rohoni ndiyo yanayotupa ufahamu wa kujua mpango wa Mungu alionao**

**nyuma ya jaribu tunalokabiliana nalo sasa. *Ebr 12: 1 – 3 (Yoh 16: 20 – 22)* yaani macho ya rohoni huiona mapema furaha inayotungoja baada ya kuvuka jaribu tunalokabiliana nalo sasa; Macho ya rohoni humwona Mungu jinsi alivyo mkuu na wa kutisha wakati adui anapotuinukia ili kututesa *2Nyak 20: 1 – 12.* Macho ya rohoni huona neema iliyo mbele ya Tanzania tofauti na majaribu wanayoyapitia Watanzania wengi leo!!**

- Kama yalivyo macho ya mwili ambayo kazi yake ni kuleta vitisho, macho ya rohoni kazi yake ni kuleta **ujasiri;** pale macho ya mwili yanapoona majitu na Wanefili, macho ya rohoni yanawaona wao ni chakula chetu **(Jaribu ndilo chakula cha jitu la imani)** ***Hesabu 13: 32 – 33, 14: 1 – 9,*** Macho ya mwilini yanaona mlima usiopandika na mambo magumu yasiyowezekana, macho ya rohoni yanaona tambarare na wepesi wa mambo; macho ya mwili yanaona vitu vinavyong'aa na kuvutia kuwa ndivyo vitu vya maana; macho ya rohoni yanaona hatari iliyonyuma ya vitu hivyo na kutozuzuka navyo!! ***Mwanzo 13: 8 – 18;*** Macho ya mwilini huona miungu na kuisujudia; macho ya rohoni humwona Mungu mkuu na wa pekee anayestahili kusujudiwa pekee!! ***Kumb 4: 7*** **(Mstari huu ndiyo unaowapa Wayahudi hata leo kutoyumba wala kutikisika baada ya kuufahamu katika roho kwamba Mungu wa Israeli ni Mungu aliye juu ya miungu yote na mataifa yote.** Na kwa kweli kabisa, kazi ya kwanza na iliyo muhimu sana kwa mwana wa Mungu baada tu ya kuokoka, anatakiwa ajazwe Roho Mtakatifu ambaye atamfungua macho yake ya rohoni ili aweze kuona mpango wa Mungu kamili ulioandaliwa kwa ajili yake na ulinzi wa Mungu ulio kwa ajili yake. ***2Wafalme 6: 16 – 17.***

3. Kuna tofauti kubwa sana kwa watu wanaosafiri kwenda mbinguni, mmoja akiongozwa na macho ya mwili huu ambao ndiyo wengi na mwingine akiongozwa na macho ya rohoni ambao ni wachache. ***2Wafal. 6: 16 – 17; Hesab 22: 21 – 35; Luk 24: 13 – 35.***

- Mwana wa Mungu aliye na macho ya rohoni atayaona matatizo na majaribu yanayomkabili yakiwa na suluhisho lake (atamwona Bwana

akiwa juu ya matatizo hayo na kuyamaliza); asiye na macho haya ya rohoni bali ana ya mwilini tu atayaona matatizo na majaribu yanayomkabili na kuanza kulia na kupiga yowe!! Elisha na Gehazi; wote wamezungukwa na maadui; Gehazi haoni msaada wa aina yoyote, bali Elisha anaona magari ya moto na farasi za moto zimewazunguka pande zote!! Anamwona Bwana Yesu akiwa upande wake.

***Rumi 8: 31 – 39***

- Sauli anamwona Mfilisti Goliathi na jeshi lake na mavazi aliyovalia kuwa ni mtu wa vita ambaye Israel hawezi kupambana naye: Bali Daudi anamwona Bwana wa majeshi wa Israel asiyeshindwa na anakwenda kupambana naye na kumshinda. ***1Sam 17: 1 – 11, 31 – 58.***
- Nehemia anaambiwa maneno magumu na rafiki yake na kumtisha na kumwogopesha; lakini pale pale Nehemia anamjibu **"Mtu kama mimi nikimbie naye ni nani akiwa kama alivyo mimi atakayeingia hekaluni ili kuponya maisha yake? Sitaingia.**
- Mtu wa Mungu aliye makini na ambaye ana macho ya rohoni saa ya jaribu **anatulia** kwanza!! Watu wengi ambao wanakufa hovyo hata ajali inapotokea ni wale **wanaopaniki** hovyo badala ya kutulia. ***Neh 6: 10 – 13.***

***Note:*** **Tukiwa na macho ya rohoni; tunapata ufahamu wa kutosha sana kuhusu Yesu tuliyemwamini na nguvu zake na uwezo wake na kazi yake aliyoifanya ya ukombozi pale msalabani na ndipo tunapokuwa na uhakika wa kina kwamba kwa Yesu mambo yote yanawezekana!! Hatudanganywi kirahisi kama ambavyo Nehemia ilikuwa siyo rahisi adanganywe!!** ***Kut 14: 10 – 14;*** **na hatutatishwa hovyo hovyo na kuogopa kama ambavyo Musa hakuogopa majeshi ya Farao; na macho yetu ya rohoni yakitiwa nuru ya ki-Mungu, tutaona kwetu mbinguni jinsi kulivyo kuzuri na jinsi ambavyo kumeandaliwa vilivyo; hatutazuzuka na dunia hii mbovu ambayo mwisho wake umekaribia sana.** ***Ufun 21: 1 – 26-*** **Haleluya.**

- Mwaka mpya **2021** uwe ni mwaka wa Kanisa kuwa macho kuona mambo kwa macho ya rohoni zaidi, kujaa ufahamu wa ndani juu ya Yesu tuliyemwamini na ukuu wake na mipango yake mikubwa aliyo nayo kwa Kanisa lake ***Math 16: 18.*** Ni mwaka wa sisi kuwa macho sana na kufahamu kwa kina kwamba tangu Bwana alipotuokoa; amebadilisha na majina yetu kabisa tuliyopewa na wazazi wetu au dunia!! ***Mwanzo 17:5; Mwanzo 32: 28 (35:10), Isaya 47: 1, 62: 4, Yoh 1: 42;*** Hutaitwa tena Simoni mwana wa Yohana waliyemzoea, utaitwa Kefa (Petro au Jiwe) Hutaitwa tena Abrahamu asiye na kitu, tasa; utaitwa Ibrahimu, Baba wa watoto wengi na tajiri mno.
- Uwe ni mwaka wa kuona mambo katika mtazamo wa ki-Mungu, wa macho ya rohoni zaidi kama Daudi alivyomwona Goliathi; tukiyaona majaribu tunayokutana nayo kwa macho ya mwili tutaishia kuogopa na kupiga yowe, tuyaone mambo na majaribu yote tutakayokutana nayo kwa macho ya rohoni – **Hii ndiyo dawa kabambe ya ushindi dhidi ya vitisho vyote vya ibilisi. *Kut 14: 13 – 14* tusome tena wote.**

Bwana ampatie kila mteule macho ya moyoni kuanzia tarehe hii **01/01/202**1, auone ukuu na uweza wa Mungu katika mambo yote na hivyo aweze kusema **“Mtu kama mimi niogope kifo” naye atamwona Bwana akiwa pale pale pamoja naye. Amina**

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***01/01/2021***